



OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA
MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA KIDATO CHA KWANZA
KISWAHILI



Muda: Saa 02:30

Mei/Juni, 2026

MAELEKEZO

1. Mtihani una sehemu tatu; A, B, na C. Jibu maswali yote kutoka kila sehemu.
2. Andika jina lako kamili kwenye nafasi uliyopewa kwa ukurasa husika.
3. Tumia peni ya blue au nyeusi kuandikia na penseli kuchorea mchoro.
4. Simu na vifaa vingine vya mawasiliano haviruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.

FOR ASSESSORS USE ONLY

QUESTION NUMBER	SCORE	ASSESSOR'S INITIALS
1		
2		
3		
4		
MsomiBora.com		
8		
9		
10		
TOTAL		
CHECKER'S INITIALS		

SEHEMU A
(Alama 15%)

Jibu Maswali yote katika sehemu hii

1. i. Ili mawasiliano yawe mazuri wazungumzaji wanatakiwa kutumia _____
A) Lugha ya Kiswahili C) Lugha fasaha ☐
B) Lugha ya Taifa D) Lugha asili ☐
- ii. Neno chachandu lina silabi ngapi?
A) Tatu B) Nne C) Tano D) Tisa ☐
- iii. Ipi kati ya tungo zifuatazo si dhima ya lugha katika mawasiliano?
A) Kutambulisha utamaduni ☐
B) Kutumia mpangilio maalumu wa sauti
C) Kuunganisha watu
D) Kupashana Habari
- iv. Hamisi na Abdala walikuwa wanabishana kuhusu muundo wa sentensi.
“Mimi ninafua na wewe utaosha vyombo”Upi ni muundo sahihi wa sentesi. ☐
A) ETUWTN B) WTUWTE C) WTUWTN D) VTUWTE
- v. Ipi si dhima ya mojawapo ya kiimbo kati ya hizi zifuatazo?
A) Kubadili maana ya neno C) Kuisitiza jambo ☐
B) Kuuliza swali D) Kuonesha hisia
- vi. “Mama alinunua vyombo vizuri. Vizuri vyote viliwekwa kabatini. Mimi nilipanga vizuri”
Katika mfuatano wa sentensi hizo, neno vizuri limetumikaje?
A) Kiwakilishi, kivumishi, kielezi C) Kielezi, kiwakilishi, kielezi. ☐
B) Kivumishi, kielezi, kiwakilishi D) Kiwakilishi, kielezi, kivumishi
- vii. Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo ina makosa ya kimatamshi?
A) Kaka amefua nguo C) Osha sahani uliolia chakula ☐
B) Suedi amenunua kanga D) John amempigia mpila Asha
- viii. _____ ni neno kuanzia moja na hutoa ujumbe kamili
A) Herufi C) Silabi ☐
B) Sentensi D) Konsonati
- ix. “a, e, i, o, u” hizi ni _____
A) Irabu C) Konsonati ☐
B) Silabi D) Sentensi
- x. Neno lipi ni tofauti na mengine?
A) Sahibu C) Mwandani ☐
B) Ajuza D) Mwenzi

JINA LA MWANAFUNZ..... MKONDO.....

2. Oanisha dhana zilizopo katika Orodha A na maelezo yaliyopo katika orodha B kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi

ORODHA A	ORODHA B
i. Utambulisha wa jamii ii. Tafsida iii. Utamaduni iv. Lugha v. Mawasiliano	A. Tamathali ya semi inayoficha au kupunguza ukali wa maneno B. Ueleza mambo yatokanayo na utamaduni wa Mtanzania C. Upashanaji wa Habari au taarifa kwa njia ya mazungumzo, maandishi au ishara. D. Makubaliano ya Pamoja baina ya wazungumzaji E. Mwenendo wa maisha unaohusisha asili, mila na desturi na jadi unaotumika katika jamii fulani F. Hueleza sifa bainifu za jamii fulani G. Mfumo wa sauti za nasibu unaotumia maneno yanayosemwa na binadamu ambao huwawezesha watu wa jamii fulani kuwasiliana

ORODHA A	i	ii	iii	iv	V
ORODHA B					

SEHEMU B

(Alama 70%)

Jibu Maswali yote katika sehemu hii

3. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku

gari, mwema, wao, shambani, ili, aisee, katika, si, pikipki, kwa

- Mwanafunzi anatakiwa kusoma vitabu vingi _____ kupata maaarifa.
- _____ lake limeharibika.
- Babu anapenda kupumzika _____ bustani ya maua.
- Mtoto _____ huwaheshimu watu wote.
- Mkulima amepanda mazao mengi _____.

4. Utata unasababishwa na mambo mengi. Toa maana mbili katika maneno yafuatayo na weka mfano mmoja kwa kila maana

- i. Kanga

a) _____

b) _____

- ii. Ua

a) _____

b) _____

JINA LA MWANAFUNZI..... MKONDO.....

iii. Pamba

a) _____

b) _____

iv. Mbuzi

a) _____

b) _____

v.. kata

a) _____

b) _____

5. Mwalimu aliwauliza wanafunzi “*inawezekana kubadili nomino zifuatazo kuwa vitenzi?*” wanafunzi wote isipokuwa HAMZA wakajibu “*HAPANA*” ikiwa wewe ni Hamza thibitisha kwa ujasiri kuwa inawezekana.

i. Wimbo _____

ii. Mlo _____

iii. Kilio _____

iv. Mtoro _____

v. Umbo _____

6. Kamusi ni mojawapo ya vifaa vilivyoorodheshwa kwenye fomu ya kujiunga na kidato cha kwanza ya Shule ya Sekondari Kisangi. Je, unadhani ni kwa nini Shule imeipa umuhimu kamusi kwa mwamafunzi?

i. _____

ii. _____

iii. _____

iv. _____

v. _____

7. Ukiwa ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza. Je, una uelewa gani kuhusiana na maneno haya?

i. Kamusi _____

ii. Kiimbo _____

iii. Mkazo _____

JINA LA MWANAFUNZ..... MKONDO.....

iv. Kitomeo _____

v. Kidahizo

8. Ili mazungumzo yakamilike lazima yahusishe watu wawili au zaidi wenye sifa zinazofanana, je sifa hizo ni zipi? (Taja sifa tano).

SEHEMU B (Alama 15%)

9. Unatamani kushiriki michezo katika Shule Jirani, Lakini utaratibu wa kiuongozi, kibusara na kihekima ni kuandika barua kwa Mkuu wa Shule ili ukashiriki. Ikiwa wewe ni mtu mwenye busara na hekima andika barua hiyo kiustadi.

This image shows a full page of white paper with horizontal blue or grey ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There is no handwriting or other markings on the paper.